TANGAZO LA SERIKALI NA. 553 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 107)*

NOTISI YA MSAMAHA WA KUSAFIRISHA NGUZO NA MAGOGO YA MKARATUSI MWEKUNDU NJE YA NCHI YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Msamaha wa Kusafirisha Nguzo na Magogo ya Mkaratusi Mwekundu Nje ya Nchi ya Mwaka 2024.

Msamaha wa kusafirisha nguzo na magogo

2.-(1) Kampuni ya Lutindi Legion Limited imepewa msamaha wa kusafirisha nguzo na magogo ya mkaratusi mwekundu yanayozidi kipenyo cha sentimenta ishirini (20) kwenda nchini Ujerumani.

(2) Kiwango cha nguzo na magogo yaliyoruhusiwa kusafirishwa chini ya aya ndogo ya (1) kitakuwa kama kilivyoainishwa katika aya ya 3.

Masharti

3. Msamaha huu unatolewa kwa masharti yafuatayo:

(a) kiwango cha nguzo na magogo ya aina iliyotajwa katka Notisi hii hakitazidi elfu moja na mia saba (1700) kama ifuatavyo-
   (i) nguzo *(Eukalyptus Red Round Poles)* mia moja (100) zenye ukubwa wa 30Cm x 30Cm x 8M;
   (ii) nguzo *(Eukalyptus Red Round Poles)* mia moja (100) zenye ukubwa wa 30Cm x 30Cm x 12M;
   (iii) magogo *(Eukalyptus Red)* mia tano (500) yenye ukubwa wa 30Cm x 30Cm x 15M;
   (iv) magogo *(Eukalyptus Red)* mia tano

(500) yenye ukubwa wa 40Cm x 40Cm x 17M; na

(v) magogo *(Eukalyptus Red)* mia tano (500) yenye ukubwa wa 44Cm x 44Cm x 19M.

(b) aina hii ya nguzo, magogo na kiwango tajwa chini ya aya (a) kitasafirishwa kwenda nchini Ujerumani.

Uhalali wa msamaha

4. Msamaha huu utakuwa halali kwa kipindi cha siku mia tatu sitini na tano kuanzia siku ya kuchapishwa kwa Notisi hii.

Dodoma,
20 Juni, 2024

ANGELLAH J. KAIRUKI
*Waziri wa Maliasili na Utalii*